**SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIKA NA HUDUMA ZA MIUNDOMBINU YA TEHAMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA, MALENGO NA KAZI ZA WAKALA**

3. Kuanzishwa kwa Wakala.
4. Malengo ya Wakala.
5. Muhuri wa Wakala.
6. Kazi za Wakala.

**SEHEMU YA TATU**
**UONGOZI WA WAKALA**

7. Bodi ya Ushauri.
8. Kazi za Bodi.
9. Muda wa Bodi.
10. Vikao vya Bodi.
11. Makamu Mwenyekiti.
12. Katibu wa Bodi.

13. Kazi za Katibu wa Bodi.
14. Kuitisha vikao.
15. Akidi ya kikao.
16. Maamuzi ya Bodi.
17. Mualikwa.
18. Kumbukumbu za vikao vya Bodi.
19. Taratibu za vikao.
20. Kamati za Bodi.
21. Kujiuzulu kwa mjumbe.
22. Nafasi kuwa wazi.
23. Kasoro katika uteuzi wa mjumbe.
24. Stahiki za Wajumbe.
25. Mkurugenzi Mtendaji.
26. Kazi za Mkurugenzi Mtendaji.
27. Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji.
28. Kukasimu kwa baadhi ya kazi.
29. Idara, divisheni na vitengo vya Wakala.
30. Watumishi wa Wakala.

**SEHEMU YA NNE**
**USIMAMIZI NA RUHUSA YA MATUMIZI YA MIUNDOMBINU YA TEHAMA**

31. Taratibu za usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA.
32. Ruhusa ya matumizi.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI VYA FEDHA

33. Fedha za Wakala.

34. Bajeti.

35. Hesabu na Ukaguzi.

36. Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

37. Ada ya uwezo wa kimtandao.

38. Kuzuia ujenzi wa miundombinu binafsi ya TEHAMA.

39. Kuunganishwa kwa mtumiaji.

40. Makosa na adhabu.

41. Kanuni.

42. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAM. 15 YA 2020**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

3 Julai, 2020

# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIKA NA HUDUMA ZA MIUNDOMBINU YA TEHAMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar ya Mwaka 2020 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Ushauri ya Wakala iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria hii;

"Uwezo wa Kimtandao" maana yake ni bando inayobeba taarifa katika mfumo wa nambari kwa sekunde na ikaainishwa kama ni taarifa ya bando la kidigitali au kimawasiliano;

“Kituo Kikuu cha Kuhifadhia Taarifa” maana yake ni huduma inayojumuisha kompyuta mtandao, seva, vifaa vya kuhifadhia taarifa na vifaa vinavyohusiana navyo, kama vile mifumo ya mawasiliano, mifumo ya uhakika ya usambazaji umeme, mazingira, utaratibu na namna ya kuhifadhi, kuchakata na kusambaza kiwango kikubwa cha taarifa;

“Anuani mtandao” maana yake ni anuani ya kipekee ya nambari na herufi inayotumika kuingia kwenye kompyuta kupitia mtandao na anuani mtandao zote zilizowekwa na mamlaka husika;

“Mkurugenzi Mtendaji” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria hii;

“Serikali” maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

“Miundombinu ya TEHAMA” maana yake ni mkonga, Kituo Kikuu cha Kuhifadhia Taarifa, minara ya mawasiliano ya simu na miundombinu mengine ya mawasiliano kama itakavyoamuliwa na Waziri;

“Kuunganishwa kwa mtumiaji” maana yake ni sehemu ya mwisho katika mpangilio wa mtandao wa mawasiliano ambayo inafikia eneo la mtumiaji wa mwisho;

“Waziri” maana yake ni waziri mwenye dhamana ya mawasiliano Zanzibar;

“Kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa” maana yake ni huduma ya Kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa inayomilikiwa na Serikali;

“Ruhusa ya matumizi” maana yake ni sehemu katika miundombinu ya TEHAMA inayotumika kuunganisha watumiaji wa mwisho au kifaa kwa madhumuni ya utoaji wa huduma za TEHAMA, na ruhusa ya kujiunga inaweza kuwa katika muundo wa waya au bando.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA, MALENGO NA KAZI ZA WAKALA

Kuanzishwa kwa Wakala.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Wakala utakaojulikana kama Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar ambao kwa jina fupi utakuwa ZICTIA.

(2) Wakala, kwa idhini ya Waziri, kwa jina lake utakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kumiliki, kununua au kuuza mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia katika mkataba wowote au muamala kwa mujibu wa sheria; na

(c) kutekeleza au kufanya jambo lolote ambalo Wakala wa namna hii, kwa mujibu wa sheria, unaweza kufanya.

Malengo ya Wakala.

**4.** Malengo ya Wakala yatakuwa ni:

(a) kutoa huduma ya miundombinu ya TEHAMA yenye unafuu, endelevu, usalama na jumuishi yenye kuwezesha kutoa huduma kwa umma;

(b) kuimarisha na kuendeleza Miundombinu ya TEHAMA na huduma;

(c) kushajiisha na kuimarisha mchango wa miundombinu ya TEHAMA kwa maendeleo ya Uchumi Zanzibar; na

(d) kufanya tathimini ya kijamii na mazingira kwa ajili ya kuhifadhi na kupata ufumbuzi wa athari zinazoweza kutokea katika miundombinu ya TEHAMA kwa umma.

Muhuri wa Wakala.

**5.**-(1) Kutakuwa na muhuri wa Wakala katika muundo na aina kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Nyaraka yoyote itakayotolewa na Wakala itawekwa muhuri wa Wakala na itathibitishwa kwa sahihi ya Mkurugenzi Mtendaji au Ofisa mwengine wa Wakala aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji.

Kazi za Wakala.

**6.**-(1) Kazi za Wakala ni:

(a) kusimamia na kuendeleza miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano na huduma;

(b) kusimamia na kuendeleza Kituo Kikuu cha Kuhifadhia Taarifa Zanzibar;

(c) kusimamia na kuendeleza anuani mtandao Zanzibar;

(d) kusimamia na kuendeleza anuani mtandao ndani ya Zanzibar;

(e) kuimarisha usalama, ulinzi, uchumi na maendeleo ya miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano kibiashara;

(f) kutoa miongozo ya miundombinu ya TEHAMA Zanzibar;

(g) kupanga na kuendeleza miundombinu ya TEHAMA Zanzibar;

(h) kutoa ruhusa ya matumizi ya miundombinu ya TEHAMA kwa kampuni zote zinazotoa huduma za simu na watoa huduma za TEHAMA Zanzibar;

(i) kutoa huduma ya kuunganisha kupitia miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi zote za Serikali Zanzibar;

(j) kutoa huduma za Miundombinu ya TEHAMA;

(k) kutoa elimu kwa umma ili kukuza uelewa na upashaji wa taarifa kwa umma kupitia usambazaji wa taarifa, elimu na mawasiliano kuhusu unyeti wa miundombinu ya TEHAMA; na

(l) kutekeleza kazi nyengine zitakazojitokeza, au ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Katika utekelezaji wa kazi zake, Wakala utazingatia uzoefu wa jumla uliokubalika kwa usalama wa miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano, taratibu, fani husika au taratibu za kitaaluma na kanuni.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI WA WAKALA

Bodi ya Ushauri.

**7.**-(1) Kunaanzishwa Bodi ya Ushauri ya Wakala ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji;

(c) Mwanasheria wa Serikali Mwandamizi kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(d) Afisa mmoja Mwandamizi kutoka wizara yenye dhamana ya fedha;

(e) Mjumbe mmoja kutoka wizara yenye dhamana ya Serikali mtandao; na

(f) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Waziri, kutokana na watu ambao wenye taaluma katika fani ya uendeshaji wa mawasiliano, usimamizi wa biashara, sheria au fani nyengine zinazohusiana.

(2) Katika uteuzi wa wajumbe wawili chini ya kifungu kidogo cha (1)(f) cha kifungu hiki, Waziri atafanya mashauriano na taasisi husika na atazingatia jinsia na taaluma.

(3) Mjumbe aliyeteuliwa kuiwakilisha taasisi atasita kuwa mjumbe wa Bodi mara tu uhusiano wake na taasisi hiyo utakaposita.

Kazi za Bodi.

**8.**-(1) Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kumshauri Waziri kuhusu kusimamia miundombinu ya TEHAMA na huduma;

(b) kupendekeza kuhusu kuandaa na kupitia sera ya Wakala kwa kuzingatia malengo yake yaliyoainishwa katika Sheria hii;

(c) kushauri kuhusu uandaaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wakala na kuidhinisha bajeti ya mwaka;

(d) kuandaa taratibu za Wakala kuhusu muundo wa kitaasisi na taratibu za kazi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(e) kupendekeza kuhusu kuanzisha idara, divisheni au vitengo vya Wakala, kama hali itakavyokuwa, kwa uongozi kama ilivyoainishwa katika Sheria hii;

(f) kumshauri Waziri kuhusiana na sera, biashara ya uhakika na mipango ya uendeshaji wa miundombinu ya TEHAMA na huduma;

(g) kujadili makadirio ya bajeti, ripoti na taarifa za ukaguzi wa fedha za Wakala kutoka kwenye uongozi, kabla ya kuwasilishwa kwa Waziri;

(h) kusikiliza malalamiko ya kinidhamu ya watumishi na kupendekeza hatua muafaka ya kuchukuliwa na Waziri;

(i) kuushauri uongozi kuhusiana na malengo, shabaha na hatua za utekelezaji wa Wakala;

(j) kupendekeza ada kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Wakala; na

(k) kutekeleza kazi nyengine yoyote iliyoelezwa na Sheria hii ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya Wakala.

(2) Bila ya kuathiri kazi zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi na Wakala zitawajibika kwa Waziri, na zitafuatilia utekelezaji wa kazi za Wakala, na zitatoa mapendekezo kwa Waziri kwa kadiri itakavyokuwa.

Muda wa Bodi.

**9.**-(1) Mwenyekiti wa Bodi atashikilia ofisi kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena.

(2) Mbali na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Bodi watashikilia ofisi kwa kipindi cha miaka mitatu lakini wanaweza kuteuliwa tena.

Vikao vya Bodi.

**10.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja katika kila miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote ikihitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaongozwa na Mwenyekiti au ikiwa hayupo vitaongozwa na Makamu Mwenyekiti, na ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliopo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao.

Makamu Mwenyekiti.

**11.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mjumbe mmoja kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Katibu wa Bodi.

**12.**-(1) Kutakuwa na Katibu wa Bodi atakaeteuliwa na Bodi ambaye atahusika na usimamizi wa mambo ya Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa ana angalau shahada ya kwanza ya Sheria na awe muajiriwa wa Wakala.

Kazi za Katibu wa Bodi.

**13.** Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na atakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba:

(a) kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi zimechukuliwa ipasavyo;

(b) kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi zimehifadhiwa ipasavyo;

(c) taarifa sahihi za vikao vya Bodi zinatolewa kwa wajumbe kwa wakati;

(d) ushauri muafaka unatolewa kwa Bodi pale unapohitajika; na

(e) jambo jengine lolote kama Bodi itavyoelekeza.

Kuitisha vikao.

**14.** Vikao vya Bodi vitaitishwa na Mwenyekiti baada ya kushauriana na Mkurugenzi Mtendaji, kwa taarifa itakayotolewa kwa wajumbe kabla ya kikao.

Akidi ya kikao.

**15.** Zaidi ya nusu ya wajumbe inaunda akidi katika kila kikao cha Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

**16.**-(1) Bodi itafanya maamuzi yake kwa njia ya makubaliano na iwapo haikukubaliana, maamuzi yatafikiwa kwa kura na iwapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au mjumbe anaeongoza kikao atakuwa na kura ya maamuzi.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, maamuzi yanaweza kufanywa na Bodi kwa njia ya kusambaza nyaraka kwa wajumbe ambapo kila mjumbe ataeleza maoni yake kwa maandishi, isipokuwa kwamba mjumbe yoyote anaweza kutaka maamuzi hayo kuwasilishwa tena kwa ajili ya kujadiliwa katika kikao kamili cha Bodi.

(3) Maamuzi kwa njia ya waraka yatakuwa kwa maandishi na yaliyowekwa saini na wajumbe wote waliopo kwa wakati huo Zanzibar lakini wasipungue wajumbe watano, yatachukuliwa kuwa ni maamuzi sahihi yaliyofanywa katika kikao, isipokuwa kwamba saini ya mjumbe, ambaye jambo lake litaletwa katika kikao cha Bodi kinachofuata.

Mualikwa.

**17.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambae si mjumbe kuhudhuria majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalam lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbukumbu za Vikao vya Bodi.

**18.** Kumbukumbu za mwenendo wa kila kikao cha Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kuwekwa saini na Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Bodi.

Taratibu za vikao.

**19.** Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Bodi ina uwezo wa kuandaa taratibu zake kuhusiana na vikao na uendeshaji mzuri wa kazi zake ikijumuisha vikao vya kamati za Bodi.

Kamati za Bodi.

**20.**-(1) Bodi inaweza, kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati mbali mbali kwa kutekeleza kazi maalum kama Bodi itakavyoamua.

(2) Taratibu, masharti na mambo mengine yanayohusiana na kamati hizo zilizoanzishwa, yataamuliwa na Bodi.

Kujiuzulu kwa mjumbe.

**21.** Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Bodi anaweza, wakati wowote, kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na kwa tarehe iliyoainishwa katika taarifa au ikiwa tarehe haikuanishwa, kujiuzulu huko kutakuwa kuanzia tarehe iliyopokelewa taarifa na mamlaka ya uteuzi.

Nafasi kuwa wazi.

**22.**-(1) Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi:

(a) ikiwa amefariki;

(b) ikiwa, bila ya sababu ya msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi;

(c) ikiwa amejiuzulu au kwa njia yoyote amekosa sifa ya ujumbe wa Bodi; au

(d) ikiwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya ugonjwa wa kimwili au kiakili.

(2) Endapo mtu amesita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi, kama hali itakavyokuwa, kwa sababu yoyote ile kabla ya kumaliza muda wake, mamlaka ya uteuzi itamteua mtu mwengine kushika nafasi yake na mtu aliyeteuliwa atashikilia ofisi kwa kipindi kilichobaki cha mtangulizi wake.

(3) Endapo mjumbe yeyote hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila sababu ya msingi, Mwenyekiti wa Bodi atatoa taarifa kwa Waziri kuhusiana na jambo hilo, na Waziri atatengua uteuzi wa mjumbe huyo na atamteua mjumbe mwengine kushika nafasi yake na mtu aliyeteuliwa atashikilia nafasi kwa kipindi kilichobaki cha mtangulizi wake.

Kasoro katika uteuzi wa mjumbe.

**23.** Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kitendo au mwenendo wa Bodi hautobatilishwa kwa sababu tu ya kasoro iliyopo katika uteuzi wa mtu ambaye anapaswa kuwa mjumbe wa Bodi.

Stahiki za Wajumbe.

**24.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa stahiki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mkurugenzi Mtendaji.

**25.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya teknolojia ya habari na mawasiliano au sayansi ya komputa au fani zinazolingana na hizo kutoka chuo kikuu kinachotambulika;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka saba katika fani zilizoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) (b) cha kifungu hiki; na

(d) ana kiwango cha juu cha uadilifu na uaminifu.

Kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

**26.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala na atawajibika na usimamizi wa kazi za kila siku na kuratibu kazi za Wakala.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kazi za Wakala chini ya kifungu cha 6 cha Sheria hii, Mkurugenzi Mtendaji atahusika na:

(a) utekelezaji wa sera na programu za Wakala zinazohusiana na miundombinu ya TEHAMA na huduma;

(b) usimamizi na uendeshaji wa fedha na mali za Wakala;

(c) usimamizi na udhibiti wa wafanyakazi wa Wakala;

(d) uendeshaji na uendelezaji wa miundombinu ya TEHAMA na huduma; na

(e) utekelezaji kwa niaba ya Wakala, kazi au shughuli na kufanya jambo lolote kiuhalisia linaweza kuwa na manufaa kwa Wakala.

Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji.

**27.**- Katika utekelezaji wa kazi zilizoainishwa katika Sheria hii, Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na uwezo wa:

(a) kuandaa miongozo ya miundombinu ya TEHAMA; na

(b) kuanzisha mfumo wa mashirikiano na kukuza uhusiano baina ya wadau wa aina mbali mbali wa miundombinu ya TEHAMA.

Kukasimu kwa baadhi ya kazi.

**28.** Bila ya kuathiri sharti lolote la Sheria hii, Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukasimu kwa maandishi baadhi ya kazi zake au uwezo kwa mtumishi yeyote wa Wakala.

Idara, divisheni na vitengo vya Wakala.

**29.**-(1) Kunaanzishwa idara, divisheni na vitengo kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Waziri, kwa kushauriana na Bodi, atateua Wakurugenzi kulingana na nafasi na masharti kwa mujibu wa muundo wa taasisi ulioidhinishwa chini ya masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Meneja na Wakuu wa Vitengo watateuliwa na Mkurugenzi Mtendaji baada ya kushauriana na Bodi.

(4) Katika utekelezaji wa kazi zao, wakuu wote wa idara, divisheni na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(5) Bodi inaweza, kwa kuidhinishwa na Waziri, na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, kupendekeza kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuhusu masharti ya utumishi, ikijumuisha muundo wa motisha, muundo wa kubakiza na muundo wa utumishi kwa Wakurugenzi, Meneja, Wakuu wa Vitengo na watumishi wa Wakala.

Watumishi wa Wakala.

**30.**-(1) Wakala, kwa kuidhinishwa na Bodi, itapendekeza ajira ya watumishi wa Wakala kwa kuzingatia taratibu na masharti kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

(2) Watumishi wa Wakala waliojiriwa chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, watakuwa chini ya udhibiti na usimamizi wa Mkurugenzi Mtendaji.

## SEHEMU YA NNE
## USIMAMIZI NA RUHUSA YA MATUMIZI YA MIUNDOMBINU YA TEHAMA

Taratibu za usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA.

**31.**-(1) Bodi, kwa kushauriana na Waziri, itaandaa taratibu za usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA kuhusiana na;

(a) misingi ya uendeshaji;

(b) taratibu za biashara ya uhakika;

(c) miongozo ya matengenezo;

(d) ulazaji wa mkonga;

(e) ujenzi wa minara ya mawasiliano; na

(f) taratibu nyengine zozote kama Waziri atakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo ya Sheria hii.

Ruhusa ya matumizi.

**32.**-(1) Wakala unaweza, kwa kupitia masharti ya mkataba na kampuni za simu na watoa huduma wa TEHAMA, kuwezesha matumizi ya utoaji wa huduma zao kupitia Miundombinu ya TEHAMA iliyoainishwa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali ruhusa ya matumizi iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Wakala, kwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika, utakuwa na ruhusa ya kukagua na kuendeleza Miundombinu ya TEHAMA katika eneo lolote ikijumuisha maeneo yaliyodhibitiwa.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Wakala.

**33.** Fedha za Wakala zinajumuisha:

(a) kiwango cha fedha kilichoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika utaratibu wa ruzuku au vyenginevyo;

(b) michango halali, misaada na mikopo kama Wakala unaweza, kila baada ya muda, kupokea kutoka kwa mtu yeyote au taasisi; na

(c) fedha nyengine yoyote ambayo Wakala unaweza kuingiza au kupata, ama kwa sababu ya utekelezaji wa kazi zake au vyenginevyo.

Bajeti.

**34.** Wakala utaandaa, ndani ya miezi mitatu kabla ya kuanza mwaka mpya wa fedha, bajeti ya mwaka na utaiwasilisha kwa Waziri kwa mazingatio na kuidhinisha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Hesabu na Ukaguzi.

**35.**-(1) Wakala utaweka au utawezesha kuwekwa vitabu vya hesabu husika vya mapato na matumizi ya Wakala.

(2) Vitabu vya hesabu na kumbukumbu za matumizi zitawekwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kanuni zake.

(3) Vitabu vya hesabu vya Wakala vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu yeyote aliyemuidhinisha.

(4) Hesabu zilizokaguliwa na ripoti ya mkaguzi kuhusiana na hesabu hizo zitawasilishwa katika Bodi si zaidi ya miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha ambao hesabu hizo zinahusika kwa ajili ya kuidhinishwa.

(5) Bodi, baada ya kupokea hesabu zilizokaguliwa na ripoti kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, itaziwasilisha kama zilivyo kwa Waziri.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya fedha yaliyoainishwa katika Sheria hii, miamala yote ya fedha ya Wakala itafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka.

**36.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji, ndani ya miezi miwili baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya utekelezaji ya mwaka kuhusiana na mwaka huo wa fedha, itakayojumuisha:

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Wakala, pamoja na ripoti ya ukaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya Wakala ya mwaka wa fedha huo; na

(c) taarifa nyengine kama Waziri atakavyohitaji.

(2) Waziri atahakikisha kwamha nakala ya Ripoti ya Mwaka ya Wakala inawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi ndani ya miezi miwili au kikao kinachofuata cha Baraza la Wawakilishi baada ya kupokea ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Ada ya uwezo wa kimtandao.

**37.**-(1) Uwezo wa kimtandao kupitia miundombinu ya TEHAMA utatolewa kwa malipo ya ada kama itakavyoelezwa katika Kanuni.

(2) Mbali na ada ya uendeshaji na matengenezo, ada nyengine zilizopokelewa na Wakala katika utoaji wa huduma zake kama ilivyoainishwa katika Sheria hii zitawasilishwa katika Mfuko wa Hazina wa Serikali.

Kuzuia ujenzi wa miundombinu binafsi ya TEHAMA.

**38.** Kunazuiliwa kwa mtu yeyote, mtoa huduma za simu, mtoa huduma za mtandao au mtoa huduma za ving'amuzi kujenga miundombinu binafsi ya TEHAMA.

Kuunganishwa kwa mtumiaji.

**39.** Mtu yeyote, mtoa huduma za simu, mtoa huduma za mtandao au mtoa huduma za ving'amuzi atatumia miundombinu ya TEHAMA ya Serikali kupitia kuunganishwa kwa mtumiaji.

Makosa na adhabu.

**40.**-(1) Mtu yeyote ambaye kinyume na sheria anaharibu, anaingilia, anakata, au anafanya kitendo chochote ambacho kinasababisha hasara miundombinu ya TEHAMA, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi au adhabu zote mbili.

(2) Mtu yeyote ambaye, kinyume na sheria:

(a) anamzuia, anamkwaza au hamtii mtu yeyote wakati wa utekelezaji wa kazi au kufanya jambo lolote linalotakiwa kufanywa chini ya Sheria hii;

(b) anaharibu, anahatarisha, anavuruga au anatishia usalama au ulinzi wa miundombinu ya TEHAMA au sehemu ya miundombinu hiyo;

(c) anaingia ndani, au kwenye au anajipatisha ruhusa ya kutumia miundombinu ya TEHAMA,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

(3) Mtu yeyote ambaye ataitumia vibaya miundombinu ya TEHAMA iliyoainishwa chini ya Sheria hii, kwa lengo la kuharibu, kupotosha, kuchochea, kukashifu, kufitinisha, kudanganya au kutukana, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Hamsini lakini isiyozidi Milioni Mia Moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi lakini kisichozidi miaka ishirini au adhabu zote mbili.

(4) Endapo mtu atakwenda kiyume na sharti lolote la Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, na endapo kwenda kinyume huko hakugusi masharti ya kifungu kidogo cha (1), (2), au cha (3) cha kifungu hiki, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili.

Kanuni.

**41.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri na ufanisi wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**42.**-(1) Tangazo la Kisheria Nam. 119 la 2018 linafutwa.

(2) Kitendo chochote au jambo lolote lililofanywa chini ya Tangazo la Kisheria lililofutwa lililoanishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litachukuliwa kuwa limefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 19 Juni, 2020.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***